Shaykh Ali Hasan Al-Halabi Aijibu Kauli ya Shaykh Muhammad Bin Sa'eed Raslaan Dhidi Yake

1 February, 2014 | Posted by Salafibayaan | Refutations | 1117 views

(Haya ni makala ya Shaykh Ali Hasan al Halabi na ni jawabu lake Sheikh kwa tuhuma za Sheikh Muhammad Bin Sa'îd Raslân juu yake (Sheikh Ali).

NI NANI DR. RASLÂN:

Dr. Muhammad Bin Sa'îd Raslân ni daktari wa tiba kutoka Misri na ni khatib aliyepata umaarufu katika muda wa miaka saba iliyopita au kiasi hicho, na kabla ya wakati huo hakuwa akijulikana. Hatahivyo, katika muda huo wafuasi wake wa upofu wamefanya mbinu fulani za kumnyanyua daraja na kumfikisha kwenye nguzo ya "al-Allâmah". Haya yote yamefanyika ingawaje Raslân hakusoma kwa Sheikh yoyote, ni mtu aliyejiegemeza zaidi na kazi za mashekhe wengine na vitabu vyao vikiwa mbele yake, alikuwa zaidi akisoma kutoka kwenye vitabu na jambo lililomfanya apate umaarufu ni khutba zake za harara katika **Youtube.** Faida zilizomo katika masomo yake ni chache mno, na kiwango chake katika lugha ya kiarabu ina maana yakwamba, hatahivyo, ni watu wachache tu wanaoweza kumfahamu anayomaanisha.

Kunyanyuka kwa Raslân katika kupata umaarufu kulianza kutambuliwa na wanafunzi wa Sheikh Yahyâ al-Hajûri waliokuweko Misri. Wanafunzi hao walimtambua pindi alipokuwa akiwasifu mfano wa Sha'râwî katika khutbah zake, na jinsi alivyowekwa kuwa ni kiegemezo kama *"Sheikh wa Salafiyyah"*. Hivi karibuni Raslân alikuwa akijaribu kujipatia *Tazkiyyah* kutoka kwa Mashayekh zetu kwa da'wah yake. Hii inafafanua kugeuka kwake juu ya Sheikh Ali Hasan kama jinsi alivyofanya, bila ya kuwa na ujasiri wa kumkabili na mas'ala yake moja kwa moja pasi na kizuizi.

****

Wewe ulijiuwa mwenyewe Ewe Dr. Raslân! Haliyakuwa sisi tulikawiya wakati ambapo wewe ulipokuwa ukijiliwaza nafsi yako!

Kwahivyo ni lazima utuwiye radhi sisi!

Na hii ni iwapo utakubali hivyo au usikubali.

Ni zaidi ya mara ngapi ambapo alikuwa Sheikh wetu, Imâm al-Albâni, alikuwa akitupigia mafumbo, "Ukuta uliuambia Msumari, 'Mbona wanitoboa namna hiyo?' Msumari ukaujibu Ukuta, 'Muulize huyo anayenigonga mimi!'"

Miaka michache iliyopita tulimtembelea Dr. Muhammad Sa'îd Raslân nyumbani kwake na msikitini kwake katika mtaa anaoishi, na mimi nikatoa *Kalimah* fupi ya uongofu kwa wanafunzi wa ki-ilimu aliokuwa nao. Katika miaka baada ya kujaribu kumtembelea tena,

mahali hapohapo, kwa njia ya rafiki yake wa karibu mwenye kuheshimika, ambaye aliyesomea udaktari pamoja naye.

Lakini hata hivyo, wakati huo, ambapo ni muda wa miaka miwili iliyopita, yeye [Dr. Raslân] akatoweka, na wala sisemi kuwa “alitukimbia” kuonana na sisi, na hayo yalitokea katika kongamano la marafiki lenye baraka, ikawa ni kama sanaa ya tamthilia ya kutofaulu, ili ipate kukubalika, sisi tukalifungua fundo la dhana njema ya makosa ya njia yake, tena kwa masikitiko, mambo haya yalipata mashahidi na Allâh ni mwenye kujua, na daima akiwa ni shahidi.

Juu ya yote hayo, sisi tulijiepusha na [kuyataja] yote haya, kwani ndimi zetu saa yote hukariri, “Kwa hakika, malipo yangu yako kwa Allâh, na yeye juu ya kila kitu ni Shahidi.”

Na sisi tukamtafutia Dr. udhuru, Allâh amsamehe, mpaka tulikurubia kujidanganya nafsi zetu, [tukifikiri pengine] “labda hivi..., labda vile...” Baada ya kuwa na subira naye kwa muda mrefu, na hata mpaka tukaweka muda wa mwisho, ikadhihiri wazi yakwamba daktari wa tiba Muhammad Bin Sa’îd Raslân, twamuombea Allâh amuongoze na amtibu, hatimae sasa amekuwa ni mtu mjasiri (!) na akajifunua baadhi ya fahamu zake za ndani ambazo ndizo tulizokuwa tukizingoja, kwa kutumai, au kuwa na matumaini ya matokeo mengine yasiyokuwa haya!

Mimi nasema hapa, kwa dhihaka kiyasi fulani, “Enyi watu, hatimae Raslân amezungumza kwa ujinga na madharau, amewakejeli watu kwa maneno ya ukosefu wa adabu, haliyakuwa wao kwa hakika ni miangaza ya kumeremeta katika sehemu zao.

Alirudia maneno machafu, bila ya kustahi wala kuhusisha.

Bali kwa ujinga, [au bora kusema] kwa kufuata ki-Upofu na kuigeukia haki kando. Sisi tulikuwa tukidhania yakwamba alikuwa juu ya msimamo wa kisawasawa, lakini hata hivyo, msimamo wake uliyumbishwa.

Aliyachelewesha matapishi yake ya dhulma na urongo, na karibuni hivi yakadhihirisha wazi maana zake mbovu. Lau kama utaendelea na dhulma hii, basi ujue yakwamba kalamu za ukweli hazitodhurika, na kama aliyedhulumiwa atabakia kimya kuhusu kuendelea kuwepo, basi huwenda uliyoyasoma kutoka katika makala haya yakatosha.

Katika khutbah yake hapo jana tarehe 16th Rabee’ al-Awwal 1435 AH, akiwa juu ya minbar katika sehemu ya Subk al-Ahad, ambapo ni mahali palipojaa vichochoro na vipembe vyenye kusherehekea *bid’ah* ya Mawlid pamoja na vitendo vya ujinga vinavyotokamana na watu wasioheshimika walio na tabia mbaya.

“Miongoni mwa ma-Haddâdî- Takfîrî waliovuka mipaka ni wale wenye kushabihiyana na Rawâfidh mpaka wakawa kama wao. Unapokutana nao wakiwa wamezama [katika upotofu] wamejichagulia Taqiyyah, huu ni mfumo wa ma-Khawârij waliolaaniwa.”

Haya ndiyo aliyoyasema katika Khutbah yake iliyokosa thamani, twamuombea Allâh amuongoze. Raslân alimkusudia ‘Imâd Farâj mwenye kutushutumu sisi na mashekhe zetu juu

ya *Irjâ'* na kutubandikiza sifa za *Murji'ah* kwa ujinga na chuki. Wakati haujafika kwetu sisi kuubainisha ujinga wake, na kilicho nyuma yake na aliye nyuma yake! Kisha daktari (Raslân) akasema kwa majivuno kamili na ujasiri wa kujionyesha: *"Msingi wa madda yake ni kumuhusu Ali al-Halabi, miskîn, dhâll, ambaye mtandao wake (web site) umekuwa ni mahali pa kila sampuli ya viini vya chuki dhidi ya Sunnah na watu wake."*

Ewe Daktari Raslân:

Ni rahisi mno kwangu mimi kuyasoma yote, au kukugeuzia madai yako, wewe mwenyewe na kuyadhihirisha madai uliyoyajaza mdomoni mwako. Lau kama ningelikuwa ni wa kukuuliza wewe kuleta hata angalau chembe ya ushahidi kwa madai haya na matamshi kuhusu "upotofu", utajikuta nafsi yako huna chochote isipokuwa *taqlîd* halisi, iliyofichika kwenye khofu kubwa iliyojaa uwoga!

Wewe na hao wafuasi wa upofu nyuma yako, muko kwenye daraja moja, sasa nyinyi muna lipi la kujibu? *Wallâhi* mimi sikusema niliyoyafanya kutokana na ulaghai katika nafsi yangu, kwani "sisi twamuomba Allâh atuhifadhi kutokana na maovu ya nafsi zetu na kutokana na matokeo maovu ya vitendo vyetu", lakini hatahivyo, katika udhamini wa kumtegemea Allâh, yote ambayo unayolingania, katika tuliyokukosoa nayo katika mas'alaa ya *ghuluw* na *tajrîh* ni *udanganyifu, udanganyifu, udanganyifu!* Labda ningelikupa kidokezi, jambo ambalo (pengine huwenda) lingelikukomesha katika upande mwengine wa njia ya ukweli ambao uliokukanganya fahamu zako [daktari Raslân]

Wewe unakijua kitabu kiitwacho *'ar-Ruwât al-Mubadda'ûn min Rijâl il-Kutub is-Sunnah* (Wapokezi katika vitabu vya Sunnah Waliofanyiwa *Tabdi')*?! *Naam, naam* ndio Dr. Raslân usichaganyikiwe katika ujinga wako juu ya hilo au ghafula ukalisahau – basi hilo ni iwapo ni kweli uliyeandika ni wewe! Hii ni tasnifu iliyotarajiwa ya kitaalamu, ambayo iliyomfanya Raslân apate shahada yake ya udaktari katika ta'luma ya hadîth! Iwapo wewe Dr. Raslân umezingatia juu ya Madda ya tasnifu yako mwenyewe, kwa uadilifu, basi ungelitambua pengo kubwa baina ya Manhaj ya *ma-Imâm* wa ki-ilimu na utendeti kwenye maneno yao, na njia ya marafiki zako *ghulât* wenye kufanya *tajrih* ya kinyama na wako mbali na ukweli wa *shar'* na hukmu za Dini.

Wajuwa niliyokusudia ewe daktari Raslân? Au nizidi kukupa kamba ili pengine [wewe wajuwa namaanisha nini]? Ni kwanini uliandika kwenye Madda ya tasnifu yako "*al-Mubadda'ûn"* [Waliofanyiwa *Tabdi'*] na wala hukusema "*Mubtadi'ûn"* [wazushi]? Au hukuona/huoni tafauti yoyote baina ya hizo mbili?!

Mas'ala hapa ni: Ikiwa *ma-Imâm* wa kwanza wa *Jarh wat-Ta'dîl*, ambao walikuwa ni watu wa *taqwâ, ilm* na uadilifu, waliwafanyia *tabdi'* watu ambao hawakustahili kufanyiwa, kutokana na *Ijtihâd*, wao watalipwa wema juu ya jambo hilo kwa kuisaidia dini na kuilinda Sunnah na hadîth, na wale ambao waliowatuhumu hawatokuwa, kwa kutokana na hayo tu, "*Mubtadi'ûn"* [wazushi], watabaki tu kuwa ni "*al-Mubadda'ûn"* [Waliofanyiwa *Tabdi'*]- kwa vile wale waliowafanyia, au waliomfanyia *Tabdi'* walikosea katika *tabdi'* juu yao.

Sasa itakuwaje iwapo watu mfano wako daktari Raslân (!), wenye kujisemea kutokana na ufuasi wa upofu, upindanifu, khofu na uwoga, ili upate kujichezea mapendeleo halisi ya nafsi yako? Ewe Dr. Raslân, kitabu chako na tasnifu yako zinahitaji mkaguzi aliye muadilifu, na wala sio mfuasi wa upofu mwenye kupitisha tu, ili aweze kutoa maandiko yanayohusu misingi ya ukosoaji na uhakiki kuuhusu mfumo wako wa kujipenyeza na mabadiliko, ambao uliowanasibisha nao *Ahlul Hadîth*, haliyakuwa wao wako mbali na hayo. Mfano niliokusudia ni kama ufuatao: Aliyoyasimulia Raslân kwenye tasnifu yake, kutoka kwa wengine waliomsimulia yeye kuhusiana nayo, vol.1, Uk.615, kutoka katika maneno ya Ibn as-Swalâh katika Muqaddimah wake mashuhuri: "Zaidi ya mmoja walifanya makosa [katika ta'luma ya *Jarh wat-Ta'dil*] kuhusiana na zaidi ya mmoja, na wakawakosoa wao kwa mambo yaliyokosa misingi ya kisawasawa."

Ikiwa watu wa ta'luma hii walikuwa namna hiyo, na *taqwa* zao na uadilifu, basi wewe uko wapi na haya?

Haya yamenikumbusha katika yaliyosimuliwa na waandishi wa wasifu wa Sheikh ul-Islâm Ibn Taymiyyah (رحمه الله) alipokuwa na majadiliano na Abû Hayyân an-Nahawî kumuhusu Sibawayh. Ibn Taymiyyah alimkosoa Sibawayh na kutokana na hilo, Abû Hayyân akamsusiya Ibn Taymiyyah utadhani lilikuwa ni dhambi lisilosamehewa! Alipoulizwa Abû Hayyân kuhusu jambo hilo, alisema; "Sababu ni kwamba nilijadiliana na Ibn Taymiyyah kuhusu suala fulani linalohusiana na lugha ya kiarabu, kisha mimi nikamwambia alivyosema Sibawayh na Ibn Taymiyyah akanijibu kwa kusema, 'Sibaway si Mtume wa *nahwu*! Yeye hakuwa ni mtakatifu asiye na dhambi! Bali, aliwahi kukosea katika mas'ala 80 kwenye kitabu chake ambayo wewe huwezi kuyafahamu.'"

Ni kana kwamba sisi vilevile tunajadili mambo ambayo "wewe huyafahamu", kwahivyo, daktari Raslân hebu turudi zetu kwenye tuliyokuwa tukijadiliana.

Ama kuhusu neno "miskîn" basi ni nani huyo aliye huru kutokana na neno hilo katika mahala pake pa hakika kwa kila mwenye kulistahiki neno hilo bila ya shaka. Kwa hakika, "miskîn" ni yule atakaekuja na maneno machafu kutokana na nafsi yake akihisi kutishwa ndani yake, akawa anazungumza kwa jeuri kutokana na ujinga wa watu wa *taqlid*.

"Miskîn" si mtu asiyeogopa vitisho au akawa dhaifu mbele ya kivutio chenye ushawishi kisichoheshimika. Na *dhâl* ni mwenye kumiliki hati za vyuo vikuu (!) ambazo kwa hakika zinathibitisha kujikomboa kwake kutokana na 'ilmu inayodai na uchunguzi inayojivunia nayo! Mwenye kubadilika, kwa kutokana na matokeo ya msukumo aliolemezwa juu yake na kushindwa kuwa na subira nayo, kwa ikhtilafu na *taqlid* zinazotokamana na uovu halisi na khofu zenye kuashiriya mambo yasiyokuwa na thamani ambayo watu watwevu huyashindaniya.

Omba msamaha Ewe daktari Raslân.

Huu ni ukweli usiofaa kufichwa. Kwahivyo wacha niyaangazie mas'ala mengine.

Ama kuhusu “ukumbi wa” Ali al-Halabi, basi ni, kwa yoyote aliyeridhika nao, wacha waendelee hivyo, na yoyote mwenye kuuchukia, na waendelee kuuchukia, kwa hakika ni “ukumbi wa *ma-Salafi* wote” (kulalsalafiyeen) haki ya uhakika. Ukumbi huu uliojengwa juu ya msingi wa ilmu ambao mimi ndiye ninayeusimamia, na ambao wenye watu waliojisajili na wageni, namuomba Allâh awabariki na nyongeza kutoka katika uongofu wake, umebeba amana ya nguzo za da’wah ya salafi ambayo iko mbali na *ghuluw* na *taqsîr*. Hii ni da’wah ya uongofu tuliyoachiwa na *ma-‘Ulamâ’* wetu wema na *Mashayekh* wakubwa. Da’wah hii ambayo kurasa zake zilizotakata zimebadilishwa na nguzo zilizozuliwa na njia.

Ama kuhusu ukumbi wenyewe kuwa ni “mahali pachafu pa tuhuma”, kama yalivyokuja kutoka kwenye mdomo wa daktari Raslân, basi hii ndiyo itakuwa ni hali ya kila ambaye aliyeathiriwa kwenye macho yake na kutiwa sumu kwenye masikio yake. Ama kuhusu ukumbi kuwa ni, *“mahali pa kila sampuli ya viini vya chuki dhidi ya Sunnah na watu wake”* basi hakuna jawabu la urongo huu na udanganyifu isipokuwa tunasema:

- Waliojisajili katika ukumbi wetu ni zaidi ya 12,000
- Idadi ya madda ni zaidi ya 45,000
- Idadi ya Maudhui yaliyojadiliwa ni zaidi ya Milioni 4

Na yote haya yamekuwa ndani ya muda wa miaka 5 ya ‘ilmu, utafiti, majadiliano, Misingi, utendeti na ukosoaji, *alhamdulillâh* na twamuomba Allâh atupe msimamo katika Uislamu na Sunnah. Jee, taarifa hii haikustaajabishi, Ewe mfuasi wa Upofu (Raslân)! Kisha taarifa hii haikufurahishi ewe mwanafunzi wa ‘ilmu. Kwahiyo, ewe Raslân usingurume kwa urongo wako, chuki zako zimekuregelea mwenyewe.

Ama kuhusu Raslân kusema yakwamba ukumbi huu una “chuki dhidi ya Sunnah na watu wake”, basi *Wallâhi* hii ni njia ya watu wa *tajrîh*, wenye kuwatuhumu watu juu ya matamanio yao wenyewe halisi pasi na ‘ilmu au kutafakari, hawa ndiwo kwa hakika wenye “chuki dhidi ya Sunnah na watu wake”, na wakaweza, kwa njia ambazo hata *ma-Hizbî* na *ma-Takfiri* wenye chuki hawawezi, kuikata da’wah as-Salafiyyah na walinganizi wake wakweli. Historia ndiyo shahidi mzuri zaidi ya mambo haya. Mfano wa dhulma hii ya ujumla imerudiwa tena na Dr. Raslân, amesema: *“Ama kuhusu Ali al-Halabi, basi ni juu yake atubie kwa Allâh kwa kufungua ukumbi wa Takfiri na anatakiwa arudi kwenye Sunnah na ajue yakwamba Misri inayomfungulia mikono yake kila mara akija katika kila mwaka na imkabili mbele ya uso wake na impige kofi katika kikosi chake.”* [Hii ndiyo *tarbiya* anayovuna daktari huyu mjinga wa tiba aliyegeuka na kuwa “allâmah”?!]

Ama kuhusu *“kutubia kwa Allâh”* basi hili ndilo ninalotafuta usaidizi kutoka kwa Allâh, kadiri ya uwezo wangu, ambalo mola wetu peke yake ndiye mjuzi. Ama kuhusu *“kutubia”* kutokana na *“kufungua ukumbi”,* ndilo jambo pekee analoliota daktari Raslân, basi laa! Tena mara elfu moja laa! Litawezekana vipi hili, haliyakuwa ukumbi wenyewe ni wa mambo mema ninayofanya ili nipate kujikurubisha kwa Allâh na kuisaidia Sunnah, na kuwatetea watu wa Sunnah, licha ya pua zao.

Madai yake yakwamba ati ukumbi umefunguliwa kwa ajili ya *ma-Takfiri* ni katika madai yake mengine ya urongo, na *Wallâhi* lau kama wewe Raslân ungelikuwa na angalau chembe ya

‘ilmu ya ukumbi huo, basi ungelikimbilia kuleta taubah kabla hujafa na ukajuta kwa uliyoyasema. Ametukashifu na mambo yaliyo kinyume cha ukweli. Ama *kuhusu “kurudi kwenye Sunnah”* basi mwanzo mimi sijawahi kuiwacha Sunnah na *istiqâmah* iko kwenye mikono ya Allâh.

Ama kuhusu maneno yake yakwamba: *“na ajue yakwamba Misri inayomfungulia mikono yake kila mara akija katika kila mwaka na imkabili mbele ya uso wake na impige kofi katika kikosi chake.”* Haya ni maneno yaliyoniathiri sana, karibu yanifanye nikalia, na sio kwa ajili yangu binafsi wala sio kwa kishogo changu kupigwa kofi (!) bali, machozi kwa ajili ya Misri ambayo mfano wa dhalimu huyu (Raslân) anaweza kudai kuyazungumza kwa niyaba ya Misri, haliyakuwa ni nchi ya upendo na mapatano.

Ibn Khaldûn ameisifu Misri kuwa ni “mama wa ulimwengu”. Mimi namshukuru Allâh yakwamba mfano wa huyu daktari wa tiba (Raslân) yuko mbali na hatamu za utawala, na lau si hivyo basi angeleta ufisadi na uharibifu kwa mapendelewa yake ya nafsi katika dini na duniya, kiyasi ambacho Allâh anajua. Hapa kuna mfano mbele yako jinsi mtu huyu (Raslân), akiwa kwenye njama mbovu, anavyojaribu kuichochea nchi ya Misri dhidi yangu – mpaka hivi, yamefichuliwa.

Mimi nina hakika watu wa siyasa, katika mabadiliko yake matatu “Sâsâ, Sôsô, na Sîsî, ni wapole na wana ‘ilmu zaidi juu ya jinsi ya kuipeleka nchi na wageni wake kuliko mfano wa hawa watu wakaidi (kama Raslân), ambao wasioweza kutafautisha baina ya faida na madhara, bila ya kutaja kuwa na uwezo wa kuyakinisha rai ya sawa, kama ambavyo ***Asiyekuwa na kitu, hana uwezo wa kutoa***. Ni msemo mzuri ulioje uliosemwa na mmojawapo wa Salaf kama onyo na tahadhari: “Ulimi wangu ni kama mnyama mwitu, nikiufungua nakhofia kuwa utanimaliza mimi mwenyewe.” Imeswahihishwa kutoka kwa Zayd bin Aslam (رحمه الله) yakwamba alisema: “Abû Dujânah aliwahi kutembelewa pindi alipokuwa mgonjwa, akasema: “Mimi sina matendo yoyote niliyoyategemea kuwa ni ya uaminifu zaidi ya mambo mawili; sikuwahi kuzungumza kuhusu mambo yasiyonihusu na moyo wangu ulikuwa kwenye amani na Waislamu.” Na namkumbusha daktari kuhusu yaliyosemwa na Imâm na Tâbi’î Muhammad bin Sîrîn: “Sisi tulikuwa tukisema yakwamba watu wenye madhambi mengi zaidi ni wale wenye kutumia wakati wao mkubwa kutaja madhambi ya watu wengine.”

Sasa jicho linaweza kuuona ukweli yakwamba wewe (Ewe Raslân) sasa unafuata njia hii kwa vile umeamua kuwaridhisha baadhi ya viumbe, ambao unaowajua wewe, na kuzuiya ndimi zao zisikuzungumze wewe kama walivyofanya katika mtandao wa anti-raslan.com. Bado fursa iko wazi kwako ya kurudi nyuma, hata baada ya fedheha zote hizi na udhalilifu, zote hizo kwa ajili ya Sheikh Rabî’! Kwahivyo mche Allâh, huu sio uume kabisa, eweRaslân.

Kuna baadhi ya nukta:

1) Mimi najua kwa yakini yakwamba wewe umekatwa kabisa na ulimwengu a nje, na sasa umebaki na kiungo cha kupita *kitumbo-nge*, jamaa zako waliokusimamia mbele yako na mbele ya macho yako, wakilibeba jina lako na kukutukuza, na ni wajanja wa hila zenye msiba mkubwa, mbali na kutaja upumbavu wao na ujinga, na wote hao wawili wanastahiki kuwepo Bimaristan! Linganisha jinsi alivyokuwa Abû Hâtim na mwanaye, na jinsi alivyokuwa Subkî na mwanaye!

2) Mimi nina uwezo tena kwa utulivu (daktari Raslân), kukugeukia juu yako nikakukashifu na kukutukana, lakini kwa sasa natosheka na kuwatahadharisha watu dhidi yako na kutaja mfano wa baadhi ya naswiha ambazo baadhi ya Salaf walizowapa watoto wao: “Kuwa na upole na waliokufanyia ujeuri, kuwa mkarimu kwa wenye kujaribu kukudhuru wewe; na daima fanya upatanishi ndiyo madda ili marafiki zako wawe salama na maadui zako watahayari.”

3) Kinachotia wasiwasi ulimi wa Raslân, anapozungumza kuwahusu ma-Salafi wengine wa Misri wenye kumpinga yeye, na mimi binafsi nimewachunguza sana, na haliyakuwa hata sijawadhulumu kwa chochote wala kuwakashifu kwa madai ya urongo ya kuwabandika majina na kuwalaani kama “*Haddâdî*”, “*Khawârij*” na “*Takfîrî*”, ingawa mimi najuwa yakwamba yeye hata hajui maana ya istilahi hizi! Hata kama atakuwa yuajuwa, jambo ambalo sidhani kuwa anajua, basi ni kama yasemavyo mashairi, ‘Ikiwa hujui basi huo ni msiba, na lau kama unajua basi ni msiba mkubwa zaidi! Mapambano ya kina (asili) ni kuhusu mambo mawili:

a. Uongozi wa watu *ma-mia* machache, ambao kwa hakika inawezekana kuwa ni *ma-kumi* , ya *ma-Salafi* kutokamana na watu wa kawaida wa Misri, ambayo ni ardhi ya Waislamu Milioni 90.
b. Kutafuta hifadha mbele ya “mshika bendera wa *Jarh wat-Ta’dîl*”, mtu ambaye “vitabu vyake vyote vina ukali wa kupita kiyasi” kwa lengo la kujipatia umaarufu!

4) Kilichomchochea Raslân ni makala ambayo yaliyokuwepo kwenye mtandao kwa jina la “Jee, Ibn Raslân Amekufuru?” Haya ndiyo aliyoyakusudia kwenye khutbah yake, haliyakuwa sisi hatuna mafungamano yoyote na makala hayo. Sasa ni kwanini wewe Raslân unatushutumu sisi na ukumbi wetu mzima kwa mambo yaliyofanywa na wengine? Naam ndio, mmojawapo wa muhusika mpya wa ukumbi, miaka mitatu iliyopita aliandika makala kwa jina la “Khiyânatul Islâm” (khiyana ya Uislamu) baada ya Raslân kuikataa katiba ya Ikhwân ya Misri, ingawaje yeye mwenyewe anajua waziwazi yakwamba anaiunga mkono katiba mpya? Makala yenyewe yalikuwa ni mafupi na ikawekewa kiungo cha mtandao chenye kuiunganisha khutbah ya Raslân, na hapa kuna baadhi ya nukta:

a. Hilo tamko la “Khiyânatul Islâm” kwenye makala hayo halikutoka kwa mwenye kuyaandika makala hayo, tamko hilo ni nukuu ya kutoka kwenye khutbah yako mwenyewe Raslân pindi ulipoikataa katiba ya Ikhwân na ukawatuhumu wao, na kila mwenye kuikubali katika, kwa kuufanyia khiyana Uislamu!

5) Makala hayo yaliwahi kujadiliwa na ndugu wengi ambapo baadhi yao wakakubali, wakakosoa na kutoa maoni yao, wakikutetea wewe na maneno yako. Sasa iweje tena wewe uwajumlishe watu? Au huyo aliyekupasha wewe habari (!) amekuficha baadhi ya mambo.

6) Ukumbi wa Kulalsalafiyeen ni ukumbi wazi wa ‘Ilm na sisi hatumzuii mtu yoyote kujadili suala lolote husika la *ki-Salafi* au kutoka kwenye utafiti – hata kama linapingana na rai zetu na *ijtihâd*. Makumi ya watu walioshuhudia haya walio-ona ushabiki wa kutia shime, urongo, *taqlîd* na ta’luma za kigaidi kwenye mikumbi kama ‘*Sahab’*, ambapo huwezi kupata madda za misingi ya ki-ilimu na nguzo za maudhui muhimu zilizo wazi, isipokuwa zikijengewa ushabiki na *taqlîd,* isipokuwa katika ukumbi wetu.

7) Nnayoyajua kukuhusu wewe kutokea wakati uliopita Ewe Raslân, pengine hata hujawahi kuuzuru ukumbi huu, licha ya kutizama kwake ukumbi huu hakutomuwajibisha yeye kutekeleza *ghusl*! Kama aliwahi kufanya hivyo (kuizuru), hata kama anaweza/hawezi, atakuta kwenye ukurasa wa mbele aya isemayo,

« مَا يَلْفِظُ مِنْ قَوْلٍ إِلَّا لَدَيْهِ رَقِيبٌ عَتِيدٌ »

“Halitamki neno (mwana-adamu) ila wapo mbele yake Raqîb na Atîd (Malaika wawili wanaandika anayoyasema mwana-adamu na anayoyafanya). [Qâf:18]

Kisha moja kwa moja baada yake, pameelezwa yakwamba kila muhusika wa ukumbi huo anachukuwa jukumu mbele ya Allâh na viumbe vyake juu ya analoandika. Sasa basi Ewe Raslân, ni kwanini unatutweka sisi madhambi ya wengine, hii si dhulma?

8) Vilevile mimi naweza kufichuwa lugha ya ukosefu wa adabu ambayo Raslân aliyotumia yenye kutaja waziwazi sehemu za siri, sehemu chafu, vyoo na vinyezi, bila ya kutaja istilahi nyengine ambazo sisi twaona haya kuwatajia kwenye kurasa hizi zilizo takatifu. Yote ambayo Raslân aliyoyataja mbele ya umati wa kwenye vitongoji tulivu vya mtaa wa *Subk al-Ahad*, na mbele ya ma-kumi machache ya wasiokuwa waarabu ambao daktari Raslân amedanganyika na idadi yao na wao pia wakadanganyika na wewe Raslân kwenye ujuha mtupu, ni hali ya kusikitisha iliyoje! Hakuna mtu yoyote mwenye kukusikiliza wewe Raslân awezae kukupima uzani wako, kwahivyo usimulikwe na mng’aro!
Kubamizwa kwenye kundi dhidi yetu, katika usiyoyajua au kuyafahamu, ndio ushahidi wa mauti yako ya kweli, kwani maana ya uhai wa kweli ni aliyoyasema Allâh:

« يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اسْتَجِيبُوا لِلَّهِ وَلِلرَّسُولِ إِذَا دَعَاكُمْ لِمَا يُحْيِيكُمْ وَاعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ يَحُولُ بَيْنَ الْمَرْءِ وَقَلْبِهِ وَأَنَّهُ إِلَيْهِ تُحْشَرُونَ »

“Enyi Mlioamini! Itikieni mwito wa Allâh na wa Mtume anapowaita muamini, na jueni kuwa hapana shaka Allâh huingia kati ya mtu na moyo wake, na kwamba hapana shaka kwake yeye mtakusanywa.” [al-Anfâl: 24]

Tulikuwa na dhana njema juu yako na tulikupendelea yale ambayo tuliyojipendelea nafsi zetu, tusiwe kama ulivyotugeukia na kujitokeza mwishoni.

« وَلَكِنْ لِيَقْضِيَ اللَّهُ أَمْرًا كَانَ مَفْعُولًا لِيَهْلِكَ مَنْ هَلَكَ عَنْ بَيِّنَةٍ وَيَحْيَى مَنْ حَيَّ عَنْ بَيِّنَةٍ وَإِنَّ اللَّهَ لَسَمِيعٌ عَلِيمٌ »

“...lakini alipitisha Allâh jambo hakika ni lenye kutendeka. Ili aangamie mwenye kuangamia (akufuru mwenye kukufuru kwa ushahidi, na aamini mwenye kuamini kwa ushahidi). Na aishi mwenye kuishi kwa ushahidi, na hapana shaka Allâh ni mwenye kusikiya , mjuzi.” [al-Anfâl:42]

Kwahivyo jitahadhari Ewe daktari Raslân na usidangaywe na wale walio na sehemu katika jina lako, miongoni mwa *vitumbo nge* walio karibu yako na mbali na wewe.

Hii ni naswiha ya kihakika.
Nilikuwa ni mkali katika makala haya ili Raslân apate kuzingatia katika atakayoyasoma na arudi kwenye haki, na aje na dalili za”upotofu” huo, “viini” au *“takfiri”* na wala asijilete na maneno matupu

Ref: http://kulasalafiyyeen.com/vb/showthread.php?t=55693

Posted by Abdul Kareem Ibn Ozzie

Mfasiri Abu Farida Muhammad Awadh Salim Basawad.